Fataawaa al-Lajnah ad-Daaimah

´Abdul-´Aziyz bin Baaz
´Abdur-Razzaaq ´Afiyfiy
´Abdullaah bin al-Ghudayyaan
´Abdullaah bin Qu´uud

Tarjama na ufupisho:

Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

Juzu ya pili

YALIYOMO:

69. Kuishi Na Mume Aliyemtukana Allaah 5

70. Baadhi Ya Mambo Yenye Kumtoa Mtu Katika Uislamu 5

71. Kwanini Asikufurishwe Mwanamke Anayevaa Vibaya? 6

72. Kwanini Asikufurishwe Aliyekanusha Mambo Ya Kishari´ah? 7

73 ”Natania Tu” 7

74. Ujinga Ni Sababu Ya Kupewa Udhuru? 8

75. Wenye Kufuga Ndevu Wanafuga Kwa Kutii Amri Ya Mtume 9

76. Kuswali Nyuma Ya Anayepinga Hadiyth Swahiyh 01 10

77. Vipi Mtu Atakuwa Kafiri Ilihali Anatamka Shahaadah? 11

78. Kuswali Nyuma Ya Anayepinga Hadiyth Swahiyh 02 11

79. Kafiri Wa Kazini Kwako Ana Haki Juu Yako Ya Kumlingania 12

80. Kumfanya Mnaswara Kuwa Rafiki 12

81. Kuwatembelea Ndugu Wanaowapenda Makafiri 13

82. Kuishi Nyumba Moja Na Mshirikina 14

83. Jinsi Ya Kutangamana Na Jirani Mnaswara Na Sikukuu Zake 14

84. Kuchukua Uraia Wa Nchi Ya Kikafiri 15

85. Kafiri Kuchukua Uraia Wa Nchi Ya Kiislamu 15

86. Inafaa Kufanya Kazi Katika Mji Wa Kikafiri? 16

87. Inajuzu Kula Chakula Cha Mayahudi Na Manaswara, Kuswali Majumbani Mwao Na Kuingia Kanisani? 16

88. Siri Ya Dawa Ya Kusahau Sana Na Kupata Hifdhi Yenye Nguvu 18

89. Hapa Ndipo Itajuzu Kumkufurisha Mtu Maalum 18

90. Yeye Basi Ndiye Kafiri..... 19
91. Ahl-ul-Kitaab Ni Makafiri..... 20
92. Kusema “Dumuni Katika... “..... 20
93. “Mauti Ni Yale Yale Na Sababu Zinatofautiana”..... 21
94. Msemo “Marehemuu Fulani”..... 21
95. Ni Ipi Hukumu Ya Matamshi Haya?..... 22
96. Qiyaamah Kitasimama Baada Ya Karne Kumi Na Nne?..... 23
97. Mwenye Kudai Kuwa Mawalii Wanajua Mambo Yaliyofichikana..... 24
98. Mtu Anapokufa Malaika Wanaomchunga Hufa Pamoja Naye?..... 25
99. Mtume Alimuona Allaah Kwa Macho Ya Kichwani Mwake Usiku Wa Israa´ Na Mi´raaj?..... 26
100. Wasiwasi Wa Kwamba Mtu Anajionyesha Katika Vitendo Vyake..... 26
101. Kijana Wa Dini Anahisi Yuko London Anafanya Machafu..... 27
102. Huyu Ndiye Aliyefanikiwa..... 28
103. Taarif Ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah..... 28
104. Hawa Ndio Firqat-un-Naajiyah..... 29
105. Mapote 72 Ni Ya Peponi Au Motoni?..... 29
106. Salafiyyah Ndio Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah..... 30
107. Nini Maana Ya Salafiyyah?..... 31
108. Uhalisia Wa Mambo Juu Ya Shaykh Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab..... 32
109. Baadhi Ya Vitabu Mufiydah Vya Tawhiyd Na ´Aqiydah..... 32
110. Mapote Mengi Ya Suufiyyah Yana Bid´ah..... 33
111. Ni Kweli Walii Baada Ya Kuzikwa Kupandishwa Mbinguni?..... 34
112. Maulidi Ya Mtume Na Ya Waja Wema Yanayofanywa Tanzania..... 34

113. Kukubaliana Kwa Wanachuoni Juu Ya Ukafiri Wa Qaadiyaaniyyah 36
114. Tofauti Ya Waislamu Na Qaadiyaaniyyah..... 37
115. Ibaadhiyyah Ni Pote Potofu 38
116. Kwanini Asikufurishwe Anayesema Kuwa Jibriyl Alileta Wahyi Kimakosa?..... 38
117. Kuna Tofauti Nyingi Kati Ya Shiy´ah Na Ahl-us-Sunnah 39
118. al-Lajnah ad-Daaimah Kuhusu Shiy´ah Ithnaa ´Ashariyyah 39
119. Maana Ya Bid´ah Na Baadhi Ya Mifano Yake..... 40
120. Anayelingania Katika Sunnah Anaitwa Kuwa Ni Mfitinishaji? 41
121. Kusoma Qur-aan Kwa Pamoja Baada Ya Swalah Za Faradhi 42
122. Kusoma Qur-aan Kwa Pamoja Siku Ya Ijumaa..... 43
123. Kukusanyika Kusoma Qur-aan Kwa Ajili Ya Kupata Baraka Kazini 43
124. Kualika Watu Wasome Qur-aan Ili Mtu Anyookewe Na Mambo Yake 44
125. Kusoma Qur-aan Ijumaa Kabla Ya Imamu Kuingia Ni Bid´ah 46
126. Kukhusisha Kufanya Matendo Maalum Rajab..... 46
127. al-Lajnah ad-Daaimah Kuhusu Swawm Rajab Na Sha´baan..... 47
128. al-Faatihah Baada Ya Kuomba Du´aa Ni Bid´ah..... 48
129. Kusoma al-Faatihah Kabla Na Baada Ya Mambo Mbali Mbali Ya ´Ibaadah 49
130. al-Faatihah Baada Ya Swalah Za Faradhi..... 50



69. Kuishi Na Mume Aliyemtukana Allaah

Swali 69: Katika mji wetu kuna ada ilioenea ya dhambi kubwa ambayo ni kutukana dhati ya Allaah. Ni ipi hukumu ya Uislamu kwa hili? Je, mke mwenye kufanya hivi atalikiwe ilihali hakubali hili?

Jibu: Kutukana dhati ya Allaah ni dhambi kubwa kabisa, bali ni kuritadi kutoka katika Uislamu. Ni wajibu kwa mwenye kutumbukia katika hilo akimbilie kuleta tawbah na msamaha. Vilevile akithirishe kufanya matendo mema. Akitubu tawbah ya kweli Allaah atamsamehe na mke wake atakuwa katika ulinzi wake kwa kutubia kwake.[1]

70. Baadhi Ya Mambo Yenye Kumtoa Mtu Katika Uislamu

Swali 70: Ninakuomba unitajie hali zote ambazo zinamkufurisha mtu na kumtoa katika Uislamu na hukumu ya kafiri huyu, kuritadi, kufuru ndogo, kupenda kwa ajili ya Allaah na kuchukia makafiri kwa ajili ya Allaah.

Jibu: Mambo yenye kukufurisha ambayo yanamtoa mtu katika Uislamu ni mengi. Miongoni mwayo ni kukanusha kitu ambacho kinajulikana fika kuwepo kwake katika Uislamu. Katika mambo hayo ni kama kukanusha uwajibu wa swalah, zakaah, swawm, hajj na mfano wake. Vilevile kuhalalisha kitu ambacho kinajulikana fika uhalali wake katika Uislamu. Katika mambo hayo ni kama zinaa, kunywa pombe, kuua nafsi kwa kukusudia pasi na haki, kuwaasi wazazi wawili na mfano wa hayo. Miongoni mwa mambo hayo pia

[1] Uk. 11 fatwa 9843

kunaingia kumtukana Allaah, Mtume Wake, Uislamu, Malaika na mfano wa hayo. Kuhusu kwa kina zaidi rejea katika milango yenye kuzungumzia hukumu ya mwenye kuritadi katika vitabu vya Fiqh ili uweze kujua.[2]

71. Kwanini Asikufurishwe Mwanamke Anayevaa Vibaya?

Swali 71: Je, inajuzu kwetu kuamini kufuru ya wanawake waliovaa lakini bado wako uchi kutokana na kauli yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Hawatoingia Peponi na wala hawatonusa harufu yake... "?

Jibu: Ambaye ataamini kuwa ni halali katika wao anakufuru baada ya kubainishiwa na kumjuza hukumu. Asiyehalalisha hilo katika wao, lakini akatoka amevaa lakini bado yuko uchi, sio kafiri. Lakini hata hivyo amefanya dhambi kubwa. Ni wajibu kujivua nayo na kutubia kwayo kwa Allaah. Huenda Allaah akamsamehe. Akifa juu ya dhambi hiyo kabla ya kutubia yuko chini ya matakwa ya Allaah kama watenda madhambi wengine wote. Allaah (´Azza wa Jall) anasema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ

"Hakika Allaah hasamehi kushirikishwa; lakini anasamehe yasiyokuwa hayo kwa Amtakae." (04:116)[3]

[2] Uk. 11-12 fatwa 7503

[3] Uk. 16 fatwa 8487

72. Kwanini Asikufurishwe Aliyekanusha Mambo Ya Kishari´ah?

Swali 72: Kuna mtu ni muislamu kwa baba na mama lakini hata hivyo amekataa swalah, swawm na mambo mengine katika Shari´ah ya Allaah. Je, inajuzu kutangamana naye matangamano ya waislamu kwa mfano muislamu kula pamoja naye na mengineyo?

Jibu: Hali ya mtu huyu ikiwa ni hii uliyotaja, ya kukataa swalah, swawm na mambo mengine ya Shari´ah ya Uislamu, ni kafiri kufuru yenye kumtoa katika Uislamu kutokana na kauli sahihi katika kauli za wanachuoni. Anatakiwa kuambiwa kutubia kwa siku tatu, akitubu ni sawa, la sivyo mtawala wa waislamu amuue kama wanavyouawa wenye kuritadi.

Haijuzu kwa waislamu kumpenda, kumtembelea na kadhalika. Isipokuwa ikiwa kama itakuwa ni kwa lengo la kumnasihi na kumwelekeza na kumuadhisha. Huenda akatubu kwa Allaah (Subhaanah).[4]

73 "Natania Tu"

Swali 73: Baadhi ya watu wanazungumza maneno ambayo yanaweza kuwa yanawapelekea katika kufuru au ufuska na huku anasema kuwa anafanya mzaha. Je, mzaha wake ni sahihi kumfanya asiwe na dhambi au sivyo?

Jibu: Mizaha [katika dini] imeharamishwa makatazo makubwa kutokana na ima kufuru inayopatikana ndani yake au dhambi kubwa. Allaah (Ta´ala) amesema:

وَلَئِن سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ ۚ قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُم بَعْدَ إِيمَانِكُمْ

[4] Uk. 32 fatwa 6899

"Na ukiwauliza bila shaka watasema: "Hakika tulikuwa tunaporoja na tunacheza." Sema: Je, mlikuwa mnamfanyia istihizai Allaah na *Aayaat* Zake na Mtume Wake?" Msitoe udhuru. Mmekwishakufuru baada ya kuamini kwenu." (09:65-66)

Ni wajibu kutubu kwa kitendo hicho na kuomba msamaha. Huenda Allaah akamsamehe aliyefanya hivo.[5]

74. Ujinga Ni Sababu Ya Kupewa Udhuru?

Swali 74: Je, kila mwenye kufanya kitendo cha kufuru au shirki anakufuru? Pamoja na kwamba amefanya kitendo hichi kwa kutokujua. Je, anapewa udhuru kwa ujinga au hapewi? Je, ni zipi dalili juu ya kupewa udhuru au kutopewa udhuru?

Jibu: Ambaye ´ibaadah inamuwajibikia hapewi udhuru kwa kumuabudu asiyekuwa Allaah, kujikurubisha kwa kichinjwa kwa asiyekuwa Allaah, kuweka nadhiri kwa asiyekuwa Allaah na ´ibaadah nyenginezo kama hizo ambazo ni haki ya Allaah Pekee. Isipokuwa ikiwa kama atakuwa katika mji usiokuwa wa Kiislamu na hakufikiwa na Da´wah. Katika hali hii atapewa udhuru kwa kutofikiwa na si kwa ujinga tu. Muslim amepokea kupitia kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Ninaapa kwa Yule ambaye nafsi yake Muhammad iko Mikononi Mwake, hakuna yeyote katika Ummah huu atasikia kuhusu mimi, awe myahudi au mnaswara, kisha akafa na asiamini yale niliyotumwa nayo isipokuwa atakuwa ni katika watu wa Motoni."

[55] Uk. 32-33 fatwa 6592

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakumpa udhuru aliyemsikia. Anayeishi katika mji wa Kiislamu amesikia kuhusu Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kwa hivyo hapewi udhuru katika misingi ya dini kutokana na ujinga wake.

Kuhusiana na wale waliomuomba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) awafanyie Dhaat Anwaat ili watundike silaha zao, watu hawa walikuwa ndio karibu wametoka katika ukafiri. Waliomba tu na hawakufanya. Walichokiomba ilikuwa ni kitu kinachoenda kinyume na Shari´ah. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwajibu kwa kitu chenye kutolea dalili ya kwamba lau wangelifanya walichokiomba basi wangelikufuru.[6]

75. Wenye Kufuga Ndevu Wanafuga Kwa Kutii Amri Ya Mtume

Swali 75: Ni ipi hukumu ya kuswali nyuma ya mwenye kunyoa ndevu bali anamfanyia maskhara ambaye ameachia ndevu na anamuamrisha kuzinyoa?

Jibu: Haijuzu kufanya mzaha na mwenye kuachia ndevu zake. Ameziachia kwa ajili ya kutekeleza amri ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Linalotakiwa ni kumnasihi mwenye kufanya mzaha na kumwelekeza na kumbainishia kuwa kufanya kwake mzaha huku kumfanyia ambaye anafuga ndevu zake ni dhambi kubwa. Mwenye kufanya hivo kunachelea juu yake akaritadi kutoka katika Uislamu. Amesema (Subhaanahu wa Ta´ala):

قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُم بَعْدَ إِيمَانِكُمْ

[6] Uk. 33-34 fatwa 9257

"Sema: Je, mlikuwa mnamfanyia istihizai Allaah na *Aayaat* Zake na Mtume Wake?" Msitoe udhuru. Mmekwishakufuru baada ya kuamini kwenu." (09:65-66)[7]

76. Kuswali Nyuma Ya Anayepinga Hadiyth Swahiyh 01

Swali 76: Ni ipi hukumu ya wenye kupinga Hadiyth Swahiyh ambazo zimepokelewa katika al-Bukhaariy na Muslim kama mfano wa Hadiyth zenye kuhusu adhabu ya kaburi na neema zake, Mi´raaj, uchawi, uombezi na kutoka Motoni? Je, mtu aswali nyuma yao, kuwatolea na kuitikia Salaam au mtu awasuse?

Jibu: Wanachuoni wafanye utafiti pamoja na wao kuhusu Hadiyth hizo ili wawafahamishe usahihi wazo na maana yake. Baada ya hapo wakiendelea kuzipinga au kupotosha maandiko yazo kutoka katika maana sahihi kwa kufuata matamanio yao na kufuata maoni yao batili ni watenda madhambi makubwa (Fasaqah). Ni wajibu kuwakata na kutochanganyika pamoja nao ili kuepuka shari yao. Isipokuwa ikiwa kuchanganyika pamoja nao ni kwa ajili ya kuwanasihi na kuwaelekeza.

Kuhusu kuswali nyuma yao hukumu yake ni kama hukumu ya kuswali nyuma ya mtenda dhambi. Lililo salama zaidi ni mtu kutoswali nyuma yao. Kwa sababu baadhi ya wanachuoni wamewakufurisha.[8]

[7] Uk. 35-36 fatwa 3535

[8] Uk. 36 fatwa 6280

77. Vipi Mtu Atakuwa Kafiri Ilihali Anatamka Shahaadah?

Swali 77: Je, mtu anaweza kukufuru na mdomoni mwake anatamka "hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah"?

Jibu: Mtu anaweza kuwa kafiri mbele ya Allaah na wakati huo huo anasema "hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah". Ni kama mfano wa wanafiki ambao walitamka Shahaadah kwa ndimi zao pasi na mioyo yao kuiamini. Mmoja katika wao ni ´Abdullaah bin ´Ubayy bin Saluul na watu mfano wake.[9]

78. Kuswali Nyuma Ya Anayepinga Hadiyth Swahiyh 02

Swali 78: Ni ipi hukumu ya Uislamu juu ya kuswali nyuma ya imamu ambaye anapinga Hadiyth zilizosihi kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kama mfano wa Hadiyth ya uchawi na Hadiyth kuhusu kuteremka kwa ´Iysaa bin Maryam katika zama za mwisho?

Jibu: Mwenye kupinga Hadiyth zilizothibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kama mfano wa Hadiyth hizo mbili zilizotajwa, amekosea. Anahukumiwa dhambi kubwa (Fisq). Anaweza hata kuhukumiwa kufuru juu yake kutegemea na hali yake.[10]

[9] Uk. 38 fatwa 6460

[10] Uk. 38 fatwa 9456

79. Kafiri Wa Kazini Kwako Ana Haki Juu Yako Ya Kumlingania

Swali 79: Makafiri ambao wanafanya kazi pamoja na sisi kwenye kampuni miongoni mwa wamasihi, wahinduki na manaswara wana haki zipi juu yetu na sisi tuna haki zipi juu yao? Vipi tunaweza kutangamana nao ili tusitumbukie katika kuwapenda?

Jibu: Walinganieni katika Uislamu, waamrisheni mema na kuwakataza maovu na watendeeni wema pamoja na kuchukia ile kufuru na upotevu waliyomo.[11]

80. Kumfanya Mnaswara Kuwa Rafiki

Swali 80: Je, tunaweza kuwachukulia manaswara kuwa ni ndugu zetu kama tunavyofanya kwa waislamu bila ya kutenganisha?

Jibu: Ni haramu kuwafanya manaswara kuwa ni ndugu. Amesema (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ ۘ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

"Enyi mlioamini! Msiwafanye Mayahudi na Manaswara kuwa ni marafiki - wao kwa wao ni marafiki. Na yeyote katika nyinyi atakayefanya urafiki nao, basi hakika yeye ni miongoni mwao. Hakika Allaah Haongoi watu madhalimu." (05:51)

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ

[11] Uk. 43 fatwa 9355

"Hakika Waumini ni ndugu." (49:10)

Allaah amefanya udugu wa kikweli uko kati ya waumini. Imethibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

“Muislamu ni ndugu ya muislamu mwenzake.”[12]

81. Kuwatembelea Ndugu Wanaowapenda Makafiri

Swali 81: Je, inajuzu kuwatembelea ndugu ambao wanawapenda makafiri?

Jibu: Ikiwa yule anayewatembelea anawanasihi na kuwaelekeza katika yale waliyomo katika kuwapenda makafiri na kuwafafanulia maana ya kuwapenda waumini na kuwachukia makafiri na kuwajulisha yanayowawajibikia juu ya hilo na ya haramu na kunatarajiwa wakashikamana na dini yao na kuacha maovu waliyomo, inajuzu kuwatembelea. Bali inaweza kuwa ni wajibu juu yake kwa ajili ya kuamrisha mema na kukataza maovu. Hili ni lenye kutiliwa nguvu zaidi katika haki ya ndugu kwa kuwa kufanya hivyo ni kuunga kizazi na kufikisha Shari´ah. Ikiwa hatofanya hayo wakati atapowatembelea haijuzu kwake kuwatembelea.[13]

[12] Uk. 46 fatwa 5930

[13] Uk. 62-63 fatwa 6541

82. Kuishi Nyumba Moja Na Mshirikina

Swali 82: Je, inajuzu kuishi kwa mshirikina mwenye makuba na mwenye kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allaah?

Jibu: Haijuzu kuishi kwa mshirikina miongoni mwa watu wa makuba na anayechinja kwa ajili ya siyekuwa Allaah. Anaweza kumuathiri na kumuita katika shirki zake. Isipokuwa tu ikiwa kama atakuwa ametenzwa nguvu kufanya hivo au akaona kuna maslahi kwa kufanya hivyo ili kumlingania katika dini ya Allaah na kumwelekeza ajihadhari. Pengine kwa kufanya hivo Allaah akamwongoza na kumuelekeza katika kukubali haki.[14]

83. Jinsi Ya Kutangamana Na Jirani Mnaswara Na Sikukuu Zake

Swali 83: Vipi mtu atataamiliana na mnaswara jirani wa nyumba yangu au masomo? Je, nimtembelee na kumpa hongera kwa sikukuu yake?

Jibu: Inajuzu kutangamana na mnaswara jirani kwa kumfanyia ihsani, kumsaidia katika mambo yanayoruhusu, kumtendea wema na kumtembelea ili kumlingania katika dini ya Allaah (Ta´ala) pengine Allaah akamwongoza katika Uislamu.

Kuhusu kuhudhuria sikukuu zao na kuwapongeza kwazo haijuzu kufanya hivo. Amesema (Subhaanah):

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ

"Shirikianeni katika wema na taqwa na wala msishirikiane katika dhambi na uadui." (05:02)

[14] Uk. 63-64 fatwa 5741

Kuhudhuria sikukuu zao na kuwapongeza kwazo ni aina moja wapo ya kuwapenda ambako kumeharamishwa. Hali kadhalika kuwafanya marafiki.[15]

84. Kuchukua Uraia Wa Nchi Ya Kikafiri

Swali 84: Ni ipi hukumu ya dini juu ya mtu kubadilisha uraia wake, sawa ubadilishaji huu ikiwa ni kutoka katika mji wa kiarabu wa Kiislamu na kwenda katika mji wa kiarabu wa Kiislamu mwingine, kutoka katika mji wa kiarabu wa Kiislamu na kwenda katika mji wa kiulaya pamoja na mtu kushikamana na ´Aqiydah yake ya Kiislamu?

Jibu: Muislamu kuhamisha uraia wake kutoka katika nchi ya Kiislamu na kwenda uraia wa nchi nyingine ya Kiislamu inajuzu. Ama muislamu kuhamisha uraia wake kutoka katika nchi ya Kiislamu na kwenda katika uraia wa nchi ya kikafiri haijuzu.[16]

85. Kafiri Kuchukua Uraia Wa Nchi Ya Kiislamu

Swali 85: Ni ipi hukumu ya kafiri kuchukua uraia wa nchi ya Kiislamu?

Jibu: Kafiri kuchukua uraia wa nchi ya Kiislamu inajuzu midhali kunaaminika fitina juu yake na kunatarajiwa kheri juu yake. Lakini hata hivyo asiachwe akaishi katika kisiwa cha waarabu isipokuwa akiingia katika Uislamu. Mtume

[15] Uk. 67-68 fatwa 8691

[16] Uk. 72 fatwa 6582

(Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameusia kuwatoa washirikina katika kisiwa cha waarabu.[17]

86. Inafaa Kufanya Kazi Katika Mji Wa Kikafiri?

Swali 86: Je, muislamu kufanya kazi katika nchi ya kikafiri inajuzu? Je, kitendo cha Yuusuf kinaingia katika hili?

Jibu: Ikiwa anajiamini fitina juu ya nafsi yake katika dini yake na akawa ni mwenye kujihifadhi na ni mjuzi akitarajia kuwatengeneza wengine na manufaa yake yakawa yataenea kwa wengine na asiwasaidie katika batili, itakuwa inajuzu kufanya kazi katika nchi ya kikafiri. Miongoni mwa watu hawa kunaingia pia Yuusuf (´alayhis-Swalaatu was-Salaam). La sivyo itakuwa haijuzu.[18]

87. Inajuzu Kula Chakula Cha Mayahudi Na Manaswara, Kuswali Majumbani Mwao Na Kuingia Kanisani?

Swali 87: Baadhi ya marafiki wa kinaswara masomoni wananiita manyumbani mwao ili kuchangia nao chakula. Je, inajuzu kwangu kula katika chakula chao ikithibiti kwangu kuwa ni halali katika Shari´ah?

Jibu: Ndio, inajuzu kula kwenye chakula kinachokupa rafiki yako mnaswara, sawa kikiwa katika nyumba yake au nyumba nyingine, ikikuthibitikia kuwa

[17] Uk. 74 fatwa 6495

[18] Uk. 75 fatwa 9272

chakula hiki kwa dhati yake sio haramu au hali yake haijulikani. Kwa sababu asli ni kujuzu mpaka ithibiti dalili yenye kukataza. Kuwa kwake mnaswara sio kizuizi. Kwa sababu Allaah (Ta´ala) ametuhalalishia chakula cha Ahl-ul-Kitaab.

Swali B: Je, inajuzu kwangu kuwapa vitabu vilivyo na Aayah tukufu vyenye kuthibitisha upwekekaji wa Allaah (Ta´ala) vilivyoandikwa kwa kiarabu na kutarjumiwa maana yake kwa kingereza?

Jibu: Ndio, inajuzu kuwapa vitabu vilivyo na Aayah za Qur-aan zenye kutolea dalili juu ya hukumu, Tawhiyd na mengineyo. Ni mamoja vikawa katika lugha ya kiarabu au vimetarjumiwa maana yake. Bali unashukuriwa kwa hilo kwa kuwa kuwapa navyo ili wasome ni aina moja ya kufikisha na kulingania katika dini ya Allaah. Mwenye kufanya hivo analipwa ujira akiitakasa nia yake.

Swali C: Wakati fulani swalah inafika na mimi niko kwenye nyumba ya mmoja wao. Hivyo nachukua mkeka wao maalum na naswali mbele yao. Je, swalah yangu ni sahihi kwa vile niko katika nyumba yao?

Jibu: Ndio, swalah yako inasihi. Allaah akuzidishie hima ya kumtii na khaswa kutekeleza swalah tano kwa wakati wake. Lililo la wajibu ni kufanya bidii kuziswali katika mkusanyiko na kuimarisha kwazo misikiti kiasi na utakavyoweza.

Swali D: Wameniomba kwenda nao kanisani na nikakataa mpaka kwanza niulize juu ya hukumu ya hili. Je, inajuzu kwenda nao ili niweze kuthibitisha upwekekaji ulioko katika Uislamu na kwamba ni dini ya walimwengu na ili waweze kuitikia Uislamu? Haya na khaswa ukizingatia kuwa dini yao ni ya kinaswara na madhehebu yao ni protestanti. Wanasema kuwa katika maombi yao hawana Sujuud wala Rukuu´. Pamoja na kuwa mimi kwangu ni jambo katu katu lisilowezekana nikaingia katika dini ya kinaswara kwa idhini ya Allaah (Ta´ala).

Jibu: Ikiwa kwenda kwako nao kanisani ni kwa lengo la kudhihirisha kusameheana na usahali haijuzu. Ama lengo ikiwa ni kuwalingania katika

Uislamu na ukawa haushirikiani nao katika ´ibaadah zao na huchelei kuathirika na ´ibaadah zao, ada zao na mambo yao inajuzu.[19]

88. Siri Ya Dawa Ya Kusahau Sana Na Kupata Hifdhi Yenye Nguvu

Swali 88: Kuna muislamu amemwambia ndugu yake kuwa ni kafiri pamoja na kuwa aliyeambiwa hivyo anaswali vipindi vitano na kuswali. Ni ipi hukumu na ni ipi dawa ya kusahau sana?

Jibu: Haijuzu kwa muislamu kumpachika ndugu yake kufuru ikiwa hakufanya kitu hicho. Ni wajibu kwake kutubu na kumuomba msamaha Allaah pamoja na kumtaka radhi ndugu yake. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ametishia hilo katika Hadiyth ambazo ni Swahiyh.

Kuhusu namna ya kutibu kusahau na kuhifadhi ni kumcha Allaah (´Azza wa Jall), kudumu kwa kurejelea na kukariri vile unavyotaka kuvihifadhi. Pamoja na kumuomba Allaah akusaidie juu ya hilo. Tunamuomba Allaah akupe wewe na sisi mafanikio katika kuhakikisha yale uliyoyakusudia.[20]

89. Hapa Ndipo Itajuzu Kumkufurisha Mtu Maalum

Swali 89: Je, ni katika haki ya wanachuoni kumwambia mtu maalum ya kwamba ni kafiri na kumtuhumu ukafiri?

[19] Uk. 75-76 fatwa 3262

[20] Uk. 91 fatwa 9232

Jibu: Kumkufurisha kwa jumla ni kitu kilichowekwa katika Shari´ah. Kwa mfano mtu akasema kuwa yule mwenye kutaka uokozi kwa asiyekuwa Allaah katika mambo ambayo ni haki ya Allaah Pekee, ni kafiri. Mfano wa hilo ni kama mwenye kutaka uokozi kutoka kwa Mtume miongoni mwa Mitume wa Allaah au walii amponye au amponye mtoto wake.

Hali kadhalika kumkufurisha mtu kwa dhati yake akipinga kitu ambacho kinajulikana fika uwepo wake katika Uislamu. Baadhi ya mambo hayo ni kama swalah, zakaah au swawm. Baada ya kufahamishwa ni wajibu [kumkufurisha akiendelea kupinga]. Anatakiwa kunasihiwa, akitubu ni sawa, la sivyo ni wajibu kwa mtawala kumuua hali ya kuwa ni kafiri.

Lau kumkufurisha mtu kwa dhati yake pale kunapopatikana kitu kinachowajibisha kufuru ingelikuwa ni kitu ambacho hakikuwekwa katika Shari´ah basi kusingesimamishwa adhabu ya Kishari´ah kwa wenye kuritadi kutoka katika Uislamu.[21]

90. Yeye Basi Ndiye Kafiri

Swali 90: Tunataka kujua hukumu ya mtu asiyewakufurisha makafiri?

Jibu: Ambaye kumethibiti kufuru yake ni wajibu kuitakidi kufuru yake na kumhukumu nayo na mtawala kumsimamishia adhabu ya Kishari´ah kwa kuritadi ikiwa hakutubu.

Asiyemkufurisha ambaye kumethibiti ukafiri wake, basi yeye ndiye kafiri. Isipokuwa ikiwa kama kutakuwa na utata katika hilo. Hapo itabidi kwanza kumuondolea utata wake huyo.[22]

[21] Uk. 92 fatwa 6109

[22] Uk. 93-94 fatwa 6201

91. Ahl-ul-Kitaab Ni Makafiri

Swali 91: Je, inajuzu kwa muislamu kumwambia myahudi na mnaswara kuwa ni makafiri?

Jibu: Inajuzu kwa muislamu kumwambia myahudi au mnaswara kuwa ni kafiri. Allaah amewasifu katika Qur-aan kwa wasifu huu. Hili ni jambo linalojulikana kwa yule aliyeizingatia Qur-aan. Miongoni mwa hayo ni Kauli Yake (Ta´ala):

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ فِي نَارِ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ أُولَٰئِكَ هُمْ شَرُّ الْبَرِيَّةِ

"Hakika wale waliokufuru miongoni mwa watu wa kitabu na washirikina watakuwa katika Moto wa *Jahannam* - ni wenye kudumu humo - hao ndio waovu wa viumbe." (98:05)

Ahl-ul-Kitaab ni mayahudi na manaswara.[23]

92. Kusema “Dumuni Katika... “

Swali 92: Ni ipi hukumu ya kutumia katika Khutbah na mawaidha neno “na dumuni... ”?

Jibu: Imechukizwa kufanya hivo. Kudumu ni kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Viumbe hawadumu.[24]

[23] Uk. 94 fatwa 4252

[24] Uk. 103 fatwa 5609

93. “Mauti Ni Yale Yale Na Sababu Zinatofautiana”

Swali 93: Sentesi: mauti ni mamoja na sababu zinatofautiana?

Jibu: Ndio, inajuzu kutaabiri hivyo na hakuna neno – Allaah akitaka.[25]

94. Msemo “Marehemuu Fulani”

Swali 94: Nimesikia baadhi ya maneno ambayo yanakaririwa na baadhi ya watu. Nilikuwa nataka kujua ni upi msimamo wa Uislamu kwa maneno haya. Kwa mfano anapokufa mtu kuna wanaosema “Marehemu fulani” na ikiwa ni mtu mwenye cheo kikubwa wanasema “Fulani aliyesamehewa”. Je, watu hawa wamechungulia kwenye Ubao uliohifadhiwa na kujua kuwa fulani huyo amesamehewa na fulani mwingine amerehemewa? Imekuwa watu wanachukulia usahali kuhusiana na mambo haya. Amesema (Ta´ala) katika Qur-aan:

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَتُبَيِّنُنَّهُ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْتُمُونَهُ

"Pindi Alipochukua Allaah fungamano la wale waliopewa Kitabu: Bila shaka mtakibainisha kwa watu na wala hamtokificha.” (03:187)

Naomba mnipe fatwa.

Jibu: Kuthibiti msamaha wa Allaah kwa mtu au kumrehemu (Subhaanah) baada ya kufa kwake ni katika mambo yaliyofichikana ambayo hayajui yeyote

[25] Uk. 103-104 fatwa 7887

isipokuwa Allaah (Ta´ala). Isitoshe jengine, ni nani ambaye Allaah amemjuza hilo kupitia Malaika au Mitume Wake au Manabii Wake? Mtu kusema, mbali na hawa tuliyowataja, juu ya maiti kuwa Allaah amemsamehe au amemrehemu haijuzu. Isipokuwa tu yule ambaye kuna dalili juu yake kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Vinginevyo itakuwa ni kuvurumisha bila ya kujua. Allaah (Ta´ala) amesema:

قُل لَّا يَعْلَمُ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ الْغَيْبَ إِلَّا اللَّهُ

"Sema: “Hakuna [yeyote yule miongoni mwa] waliomo katika mbingu na ardhi ajuaye ghayb isipokuwa Allaah Pekee." (27:65)

عَالِمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا إِلَّا مَنِ ارْتَضَىٰ مِن رَّسُولٍ

"Mjuzi wa ghayb na wala Hamdhihirishii yeyote ghayb Yake. Isipokuwa yule Aliyemridhia miongoni mwa Mitume." (72:26-27)

Hata hivyo kunatarajiwa kwa muislamu msamaha, rehema na kuingia Peponi. Hii ni fadhila na rehema kutoka kwa Allaah. Anatakiwa kuombewa msamaha na rehema badala ya kuelezea juu yake kwamba ni mrehemewa na amesamehewa.[26]

95. Ni Ipi Hukumu Ya Matamshi Haya?

Swali 95: Ni ipi hukumu ya Shari´ah kwa mtazamo wenu juu ya matamshi yafuatayo:

“Allaah anajua”, “Allaah asijaalie”, “Allaah asikadirie”, “Allaah ametaka iwe” na “Allaah na Mtume Wake ndio wanajua zaidi”?

[26] Uk. 106-107 fatwa 8217

Jibu: Kuhusu "Allaah anajua" ni sawa kusema hivyo lau atakuwa ni mkweli. Kuhusu "Allaah asijaalie" na "Allaah asikadirie" ni sawa kusema hivo makusudio ya kusema hivo ni kuomba usalama kutokana na mambo yenye kudhuru. Kuhusu "Allaah ametaka iwe" ikiwa anakusudia maradhi yaliyomfika, ufukara na kadhalika ni katika makadirio na matakwa ya Allaah ya kilimwengu (Kawniyyah) ni sawa.

Kuhusiana na "Allaah na Mtume Wake ndio wanajua zaidi" inajuzu kusema hivyo wakati wa uhai wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ama baada ya kufa kwake aseme "Allaah ndiye anajua zaidi". Kwa kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hajui yanayoendelea baada ya kufa kwake.[27]

96. Qiyaamah Kitasimama Baada Ya Karne Kumi Na Nne?

Swali 96: Nimesikia baadhi ya wanachuoni wetu wakisema kuwa katika Hadiyth kuna khabari yenye kusema "Qiyaamah kitakuwa baada ya karne kumi na nne na kitu". Je, maelezo haya ni sahihi? Kwa vile kumeshapita karne kumi na nne na hakukupitika kitu.

Jibu: Hakuna anayejua kwa kulenga wakati wa Qiyaamah kitaposimama isipokuwa Allaah (Subhaanah). Hakuna katika Hadiyth Swahiyh yoyote chenye kutolea dalili juu ya usahihi wa yale aliyoyasema yule uliyemnasibishia maneno hayo.[28]

[27] Uk. 108 fatwa 10751

[28] Uk. 120 fatwa 7350

97. Mwenye Kudai Kuwa Mawalii Wanajua Mambo Yaliyofichikana

Swali 97: Allaah (Ta´ala) amesema:

عَالِمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا إِلَّا مَنِ ارْتَضَىٰ مِن رَّسُول

"Mjuzi wa ghayb na wala Hamdhihirishii yeyote ghayb Yake. Isipokuwa yule Aliyemridhia miongoni mwa Mitume." (72:26-27)

Je, walii katika Ummah wa Mtume ni mwenye kuwafuata kwa kujua mambo yaliyofichikana?

Jibu: Allaah (Subhaanah) amehukumu kuwa elimu ya mambo yaliyofichikana ni jambo maalum Kwake. Amesema:

قُل لَّا يَعْلَمُ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ الْغَيْبَ إِلَّا اللَّهُ

"Sema: “Hakuna [yeyote yule miongoni mwa] waliomo katika mbingu na ardhi ajuaye ghayb isipokuwa Allaah Pekee." (27:65)

Hakuvua katika hilo isipokuwa Aliyemridhia miononi mwa Mitume ndiye ambaye anamdhihirisha yale anayoyataka katika mambo yaliyofichikana. Allaah (Ta´ala) amesema:

عَالِمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا إِلَّا مَنِ ارْتَضَىٰ مِن رَّسُول

"Mjuzi wa ghayb na wala Hamdhihirishii yeyote ghayb Yake. Isipokuwa yule Aliyemridhia miongoni mwa Mitume."

Mwenye kudai kuwa kuna mtu katika Ummah wa Manabii na wa Mitume ya kwamba anajua mambo yaliyofichikana ni mwongo. Mwenye kudai kuwepo

yeyote katika mawalii na watu wema, ambao ni wafuasi wa Mitume katika imani na matendo, kwamba anajua mambo yaliyofichikana ni mwenye kusema uongo. Anakadhibisha yaliyoteremka katika Qur-aan na Hadiyth zilizothibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) zenye kufahamisha kuwa elimu ya mambo yenye kufichikana ni mambo maalum yenye kujua Allaah.[29]

98. Mtu Anapokufa Malaika Wanaomchunga Hufa Pamoja Naye?

Swali 98: Tufutie juu ya Malaika wenye kuwakilishwa kwa mwanaadamu juu ya kuyadhibiti matendo yake katika kipindi cha uhai wake, nao ni "Raqiyb" na "´Atiyd". Wakati mtu anakufa Malaika hawa na wao wanakufa pamoja naye? Ni wapi yanakuwa mafikio yao baada ya mtu kufariki?

Jibu: Hali za Malaika na kazi zao ni katika mambo yaliyofichikana. Hayajulikani isipokuwa kwa kuwepo dalili katika Qur-aan na Sunnah. Hakukuthibiti dalili juu ya kufa kwa Malaika mwenye kuandika mema na maovu wakati anapokufa yule ambaye wamewakilishwa juu yake ili kuandika mema na maovu yake kama ambavyo vilevile hakuna dalili juu ya kwamba wanaendelea kuishi na mafikio yao ya mwisho. Hilo linajua Allaah Pekee. Hayo yaliyoulizwa sio katika mambo ambayo tumewajibishiwa kuyaamini na hayahusiani na matendo. Hivyo kuuliza juu ya mambo hayo ni kuingia katika kitu kisichokuhusu. Kwa hivyo tunamnasihi muulizaji asiingie katika kitu kisichomuhusu. Atumie bidii zake kuuliza juu ya mambo ambayo yatamletea yeye na waislamu manufaa katika dini na dunia yao.[30]

[29] Uk. 120-121 fatwa 3502

[30] Uk. 124 fatwa 41

99. Mtume Alimuona Allaah Kwa Macho Ya Kichwani Mwake Usiku Wa Israa´ Na Mi´raaj?

Swali 99: Je, Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimwona Mola Wake (Ta´ala) usikuwa Israa´?

Jibu: Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakumwona Mola Wake duniani kwa macho ya kichwani mwake kutokana na kauli sahihi ya wanachuoni juu ya hilo. Alimwona Jibriyl (´alayhis-Salaam) kwa umbile lake kwenye upeo angani. Haya ndio makusudio ya Kauli Yake (Ta´ala):

عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَىٰ

"Amemfunza aliye mwingi wa nguvu... " (53:05-17)[31]

100. Wasiwasi Wa Kwamba Mtu Anajionyesha Katika Vitendo Vyake

Swali 100: Mimi naswali, nafunga, nasoma Qur-aan na napambana ili niweze kutekeleza maamrisho ya Qur-aan na Sunnah. Lakini hata hivyo napata hisia za kwamba sifanyi haya isipokuwa ili kusemwe "huyu ni mtu wa dini". Hisia hizi zinaweza kunifanya kuacha kufanya mambo fulani kwa kuchelea. Vipi nitajinasua na hili?

[31] Uk. 130 fatwa 5611

Jibu: Ni juu yako kutekeleza maamrisho ya Uislamu kwa kujisalimisha na maamrisho ya Allaah na kutaka thawabu zake. Puuzia wasiwasi unaokujia juu ya kwamba matendo yako haya ni kujionyesha. Pambana na wasiwasi huo kiasi na utakavyoweza.[32]

101. Kijana Wa Dini Anahisi Yuko London Anafanya Machafu

Swali 101: Mimi ni kijana mwenye umri wa miaka 19. Namshukuru Allaah kuona naswali swalah tano zote msikitini kwa mkusanyiko ikiwa ni pamoja na Fajr. Baadhi ya nyakati naadhini msikitini na nimehifadhi karibu juzu sita. Lakini hata hivyo kuna kitu kinanipa dhiki sana, nacho ni kwamba pindi nakuwa nimekaa peke yangu au nimelala najiwa na fikra na kuwaza – na naomba kinga kwa Allaah – ya kwamba nimesafiri kwenda London, nimefanya zinaa na kukutana na wasichana waovu. Je, napata dhambi kwa hilo kwa kuzingatia ya kwamba hili haliniathiri. Hufanya punyeto ingawa ni mara chache sana. Nachelea ikanigusa Hadiyth yenye maana:

“Yule ambaye swalah yake haimzuii na machafu na maovu basi Allaah atamzidishia umbali.”

Jibu: Kwanza wasiwasi na yale yanayoelezwa na moyo muislamu haadhibiwi kwayo. Imethibiti kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah (Ta´ala) ameusamehe Ummah wangu kwa yale yanayoelezwa na nafsi zao midhali hawajayatamka.”

Pili kujitoa manii kwa mkono kitu kinachoitwa “punyeto” ni haramu.

[32] Uk. 133 fatwa 8691

Tatu Hadiyth uliyotaja ni dhaifu. Lakini maana yake inajulikana kwa kundi katika Maswahabah na Taabi´uun (Radhiya Allaahu ´anhum).

Tunataraji kuwa wasiwasi hautokushughulisha maadamu umejiepusha na maasi.[33]

102. Huyu Ndiye Aliyefanikiwa

Swali 102: Ni nani aliyefanikiwa mbele ya Allaah?

Jibu: Aliyefanikiwa ni yule aliyeshikamana barabara na dini ya Allaah na akaishika kiimani, maneno na vitendo kutoka katika Qur-aan na Sunnah kwa ufahamu wa Salaf-us-Swaalih kutoka kwa Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wenye kuwafuata kwa wema.[34]

103. Taarif Ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah

Swali 103: Ni ipi taarif ya istilahi ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah? Je, wanachuoni wa masomo ya Burayluu India wanazingatiwa ni katika Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah na kwa nini?

[33] Uk. 133-134 fatwa 7349

[34] Uk. 147 fatwa 4889

Jibu: Ni wale waliyomo katika mfano wa yale aliyokuwemo Muhammad bin ´Abdillaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah zake wote. Hawa ndio Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.[35]

104. Hawa Ndio Firqat-un-Naajiyah

Swali 104: Ni yapi maoni yako juu ya sifa ya kundi lililookoka, Firqat-un-Naajiyah? N kina nani? Ni upi mfumo wao? Ni ipi nchi yao ikiwa kama hilo limetajwa katika Hadiyth au maneno ya wanachuoni?

Jibu: Kundi lililookoka ni lile liliyoko katika mfano wa yale aliyokuwemo Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah zake. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alifasiri hivyo. Mfumo wao ni kuwa wanafuata Qur-aan na Sunnah. Hawana mji maalum.[36]

105. Mapote 72 Ni Ya Peponi Au Motoni?

Swali 105: Nimeijua Hadiyth hii tangu kitambo na naifanyia bidii iliyokuwa kubwa, nayo ni hii ifuatayo:

“Ummah wangu utafarikiana katika mapote sabini na tatu. Yote yataingia Motoni isipokuwa moja tu. Nalo ni lile lenye kufuata yale niliyomo mimi na Maswahabah zangu.”

[35] Uk. 156-157 fatwa 4143

[36] Uk. 159 fatwa 6229

Hadiyth hii siku zote niliijua hivi. Lakini hata hivyo nilikuwa nasoma baadhi ya vitabu na nikaona Hadiyth hii ikiwa na nyongeza yenye kusema:

"Yote yataingia Peponi isopokuwa moja tu."

Ninaapa kwa Allaah ya kwamba upokezi huu umenitatiza sana. Uhalisia wa mambo ni kwamba yote yataingia Motoni isipokuwa moja au yote yataingia Peponi isipokuwa moja tu?

Jibu: Matamshi yaliyothibiti katika upokezi wote uliokuja ni:

"Yote yataingia Motoni isipokuwa moja tu."

Kuhusu upokezi wenye kusema:

"Yote yataingia Peponi isopokuwa moja tu."

hauna asli yoyote.[37]

106. Salafiyyah Ndio Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah

Swali 106: Nilikuwa naomba tafsiri ya neno "Salaf" na ni kina nani "Salafiyyuun"?

Jibu: Salaf ni Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ambao ndio wenye kumfuata Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) miongoni mwa Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) na wenye kufuata uongofu wao mpaka siku ya Qiyaamah. Wakati Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipoulizwa juu ya kundi lililookoka akasema:

"Ni lile lenye kufuata yale niliyomo mimi hii leo na Maswahabah zangu."[38]

[37] Uk. 160 fatwa 7278

107. Nini Maana Ya Salafiyyah?

Swali 107: Salafiyyah ni nini na una maoni gani juu yao?

Jibu: Salafiyyah ni unasibisho wa Salaf. Salaf ni Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), maimamu wa uongofu kutoka katika zile karne tau bora za kwanza (Radhiya Allaahu ´anhum). Watu hawa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amewashuhudia wema pale aliposema:

“Watu bora ni wa karne yangu, kisha wataofuatia, kisha wataofuatia. Halafu baada ya hapo watakuja watu ushuhuda wa mmoja wao utashinda kiapo chake na kiapo chake kitashinda ushuhuda wake.”

Ameipokea Imaam Ahmad katika “al-Musnad", al-Bukhaariy na Muslim.

Salafiyyuun ni wingi wa Salaf. Salafiy ni unasibisho wa Salaf na tumetangulia kutaja maana yake. Ni wale wenye kufuata mfumo wa Salaf katika kufuata Qur-aan na Sunnah na kulingania katika vitu hivyo na kuvitendea kazi. Kwa hayo ndio wakawa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.[39]

[38] Uk. 164 fatwa 6149

[39] Uk. 165-166 fatwa 1361

108. Uhalisia Wa Mambo Juu Ya Shaykh Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab

Swali 108: Kuna baadhi ya watu wamenambia kuwa kuna Wahhaabiyyah ambapo mimi nikawaambia kuwa hakuna Wahhaabiyyah, ni madai yaliyozushwa na waovu ili kuwakimbiza watu na Da´wah yenye kutengeneza. Pamoja na hivyo kuna aliyenambia kuwa Shaykh Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab alikuwa mwema [mwanzoni] lakini mwisho mwa uhai wake alipinda kwa sababu alipinga baadhi ya Hadiyth Swahiyh za Mtume kwa vile haziafikiani na maoni yake. Unasemaje juu ya hilo?

Jibu: Shaykh Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) ni katika walinganizi wakubwa wa Salafiyyah na ´Aqiydah iliosalimika na mfumo uliyonyooka. Vitabu vyake vinatolea ushahidi juu ya hayo.

Kuhusu uliyosema kuwa mpinzani wake mmoja amesema kuwa Shaykh mwishoni mwa uhai wake alipinda kwa vile alikataa baadhi ya Hadiyth Swahiyh kwa vile haziafikiani na matamanio yake, huu ni uongo na uzushi kwa Shaykh. Shaykh amekufa hali ya kuwa ni mtu mkubwa mwenye kuziheshimu Sunnah, kuzikubali, bali sivyo tu na kulingania kwazo (Rahimahu Allaah).[40]

109. Baadhi Ya Vitabu Mufiydah Vya Tawhiyd Na ´Aqiydah

Swali 109: Ni vipi vitabu vyenye kunufaisha katika kuifahamu ´Aqiydah?

Jibu: Vitabu vyenye faida katika kuifahamu ´Aqiydah vinatofautiana kutegemea na kutofautiana kwa watu katika kuvielewa, utamaduni na daraja

[40] Uk. 173-174 fatwa 6477

zao za kielimu. Ni juu yake kumtaka ushauri mwanachuoni aliye karibu naye ambao wanajua hali yake, uwepesi wa kufahamu kwake na kujifunza elimu.

Miongoni mwa vitabu vyenye faida katika ´Aqiydah kwa njia ya kijumla ni pamoja na “al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah” na ufafanuzi wake, ufafanuzi wa “al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah”, “Kitaab-ut-Tawhiyd” cha Shaykh Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab pamoja na ufafanuzi wake “Fath-ul-Majiyd” na ufafanuzi wake mwingine “Taysiyr-ul-´Aziyz al-Hamiyd”, “Kashf-ush-Shubuhaat” na “Thalaathat-ul-Usuwl” vyote viwili hivi ni vya Shaykh Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab, “at-Tadmuriyyah” na “al-Hamawiyyah” vyote viwili hivi ni vya Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah, kitabu “at-Tawhiyd” cha Ibn Khuzaymah na Qaswiydah “an-Nuuniyyah” na ufafanuzi wake. Pamoja na kujua kuwa kitabu kikubwa na kitukufu kuliko vyote ni “Kitabu cha Allaah kikubwa”. Ndani yake mna ubainifu wa wazi kabisa juu ya ´Aqiydah sahihi na ubainifu wa yenye kuyabatilisha na kwenda kinyume nayo. Hivyo tunakuusia kukithirisha kukisoma na kuzingatia maana yake. Humo mna uongofu na nuru, uongofu juu ya kila kheri na matahadharisho juu ya kila shari. Amesema (Ta´ala):

إِنَّ هَٰذَا الْقُرْآنَ يَهْدِي لِلَّتِي هِيَ أَقْوَمُ

"Hakika hii Qur-aan inaongoza katika yaliyonyooka kabisa." (17:09) [41]

110. Mapote Mengi Ya Suufiyyah Yana Bid´ah

Swali 110: Ni ipi hukumu ya mapote ya Suufiyyah ya leo?

[41] Uk. 175-176 fatwa 3863

Jibu: Mapote mengi ya Suufiyyah yana Bid´ah. Tunakunasihi kufuata uongofu wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah zake katika ´ibaadah na mambo mengine. Soma kitabu "Haadhihiy hiya as-Suufiyyah" cha ´Abdur-Rahmaan al-Wakiyl (Rahimahu Allaah).[42]

111. Ni Kweli Walii Baada Ya Kuzikwa Kupandishwa Mbinguni?

Swali 111: Je, ni sahihi yale yanayosemwa na watu ya kwamba walii akifa na kutiwa ndani ya kaburi anajiwa na Malaika wanamtoa ndani ya kaburi hilo na kumpandisha mbinguni?

Jibu: Hilo si sahihi. Kinachopandishwa ni roho na inafunguliwa milango ya mbinguni akiwa muumini au anafungiwa nayo akiwa ni kafiri. Kisha baada ya hapo inarudishwa ardhini.[43]

112. Maulidi Ya Mtume Na Ya Waja Wema Yanayofanywa Tanzania

Swali E: Sisi Tanzania tunatengeneza chakula na tunakusanyika sehemu maalum ndani ya nchi na tunasema kuwa matembezi haya yanatokamana na mtu fulani kutoka katika pote la Qaadiriyyah ambaye ni ´Abdul-Qaadir. Je, kitendo hichi ni katika Bid´ah au ni katika Sunnah ya Mtume wa Allaah

[42] Uk. 185 fatwa 6433

[43] Uk. 7781

(Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)? Je, kina madhambi? Kwa sababu hatuimarishi misikiti mpaka kwanza kufanywe matembezi haya na kusoma Maulidi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa kufanya sherehe kubwa kwa sababu hiyo. Je, mambo haya yana madhambi au hapana?

Jibu: Katika zama za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), Maswahabah zake na Salaf-us-Swaalih hakupatapo kufanywa walima wala chakula juu ya maiti mwema aliyefariki. Hakuna Swahabah yeyote wala Salaf-us-Swaalih aliyesherehekea Maulidi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika uhai wake wala baada ya kufa kwake. Vilevile hawakufanya chakula baada ya kufa kwake.

Kwa hivyo kufanya Maulidi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), mtu mwema miongoni mwa watu wema au viongozi, mtu akasherekea hilo, kukasomwa yaliyoandikwa wakati wa kuzaliwa kwake, waliohudhuria wakasimama wakati kunapotajwa mazao yake kwa madai ya wenye kuhudhuria ya kwamba [mtu huyo] amekuja katika wakati huo, kufanya chakula kwa ajili ya kusherehekea Maulidi ya Mtume, Shaykh ´Abdul-Qaadir au mtu mwingine ni miongoni mwa Bid´ah za maovu.

Kumheshimu Mtume na kumpenda inakuwa kwa kumfuata yeye na Shari´ah yake Allaah (Ta´ala) amesema:

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

"Sema: “Mkiwa mnampenda Allaah, basi nifuateni Atakupendeni Allaah na Atakughufurieni dhambi zenu." (03:31)

Kuwaheshimu watu wema na kuwapenda inakuwa kwa kuwafuata katika yale yenye kuafikiana na uongofu wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Sunnah zake.

Lililo la wajibu kwa waislamu ni wao washikamane na Sunnah za Mtume wao na Sunnah za makhaliyfah waongofu baada yao na mapokezi yao. Sambamba

na hilo watahadhari na kuvuka mipaka kwa watu wema na kuwasifu kwa kupindukia. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Msinisifu kwa kupitiliza kama jinsi manaswara walivyofanya kwa mwana wa Maryam. Hakika mimi ni mja. Hivyo semeni “Mja wa Allaah na Mtume Wake”.”

Ameipokea al-Bukhaariy katika “as-Swahiyh” yake.

Amesema tena (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

“Tahadharini na kuvuka mipaka katika dini. Hakika kilichowafanya kuangalia waliokuwa kabla yenu ilikuwa ni kuvuka mipaka.”[44]

113. Kukubaliana Kwa Wanachuoni Juu Ya Ukafiri Wa Qaadiyaaniyyah

Swali 113: Ninatarajia kutubainishia hukumu ya Uislamu juu ya kundi la Qaadiyaaniyyah na Mtume wao wa uongo Ghulaam Ahmad al-Qaadiyaaniy. Vilevile tunaomba kututumia kitabu chochote kinachozungumzia kuhusu kundi hili kwa vile mimi nina hamu ya kulisoma.

Jibu: Utume umekhitimishwa kwa Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hivyo hakuna Mtume mwingine baada yake. Hilo limethibiti katika Qur-aan na Sunnah. Mwenye kudai utume baada ya hapo ni mwongo. Miongoni mwa watu hao ni Ghulaam Ahmad al-Qaadiyaaniy. Kudai kwake utume ni uongo. Wafuasi wake waliodai kwamba ni ukweli ni madai ya uongo.

[44] Uk. 198-202 fatwa 948

Kikao cha baraza la wanachuoni wakubwa Saudi Arabia wamethibitisha kuwa Qaadiyaaniyyah ni kundi la kikafiri kwa ajili ya hilo [kudai kwao utume].[45]

114. Tofauti Ya Waislamu Na Qaadiyaaniyyah

Swali 114: Ni ipi tofauti kati ya waislamu na Ahmadiyyuun/Qaadiyaaniyyuun?

Jibu: Tofauti kati yao ni kuwa waislamu ni wale wanaomuabudu Allaah Pekee na wanamfuata Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Vilevile wanaamini kuwa yeye ndiye Mtume wa mwisho na hakuna Nabii mwingine baada yake.

Ama kuhusu Ahmadiyyuun ambao ndio wafuasi Mirzaa Ghulaam Ahmad ni makafiri. Sio waislamu. Wanadai kuwa Mirzaa Ghulaam Ahmad ni Nabii baada Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mwenye kuamini imani hii ni kafiri kwa makubaliano ya wanachuoni wote wa waislamu. Allaah (Subhaanah) anasema:

مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رَّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ

"Hakuwa Muhammad baba wa mmoja yeyote miongoni mwa wanaume wenu, lakini ni Mtume wa Allaah na ni mwisho wa Manabii." (33:40)

Imesihi kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

“Mimi ndio Nabii wa mwisho. Hivyo basi hakuna Nabii baada yangu."[46]

[45] Uk. 221 fatwa 4317

115. Ibaadhiyyah Ni Pote Potofu

Swali 115: Je, pote la Ibaadhiyyah linazingatiwa ni katika mapote potevu? Je, inajuzu kuswali nyuma yao?

Jibu: Pote la Ibaadhiyyah ni miongoni mwa mapote potevu kutokana na uadui, mashambulizi na uasi kwa ´Uthmaan bin ´Affaan na ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhum). Haijuzu kuswali nyuma yao.[47]

116. Kwanini Asikufurishwe Anayesema Kuwa Jibriyl Alileta Wahyi Kimakosa?

Swali 116: Mnawahukumu vipi Shiy´ah na khaswa wale wenye kusema kuwa ´Aliy yuko katika ngazi ya utume na kwamba Jibriyl alikosea kwa kuteremka kwake kwa Muhammad?

Jibu: Shiy´ah ni mapote mengi. Wale miongoni mwao wenye kusema kuwa ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) yuko katika ngazi ya utume na kwamba Jibriyl (´alayhis-Salaam) alikosea kwa kuteremka kwake kwa Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni makafiri.[48]

[46] Uk. 221-222 fatwa 8536

[47] Uk. 260-261 fatwa 6935

[48] Uk. 266 fatwa 8564

117. Kuna Tofauti Nyingi Kati Ya Shiy´ah Na Ahl-us-Sunnah

Swali 117: Naomba uniwekee wazi tofauti kati ya Ahl-us-Sunnah na Shiy´ah na pote lililo karibu zaidi katika Sunnah?

Jibu: Tofauti zilizopo kati ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah na Shiy´ah ni nyingi katika yanayohusiana na Tawhiyd, utume, uongozi na mengineyo.

Wanachuoni wengi wameandika kuhusu hilo. Baadhi yao ni Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah katika "Minhaaj-us-Sunnah", "al-Milal wan-Nihal" cha ash-Shahrastaaniy, "al-Fiswal" cha Ibn Hazm, "al-Khutwut al-´Ariydhwah" na "al-Mukhtaswar at-Tuhfah al-Ithnaa ´Ashariyyah" vya Muhibb-ud-Diyn al-Khatwiyb. Juu ya hilo rejea vitabu vilivyotajwa.[49]

118. al-Lajnah ad-Daaimah Kuhusu Shiy´ah Ithnaa ´Ashariyyah

Swali 118: Je, pote la Shiy´ah al-Imaamiyyah ni katika Uislamu? Ni nani aliyeliunda? Shiy´ah wanayanasibisha madhehebu yao kwa ´Aliy (Karrama Allaahu wajhah). Madhehebu ya Shiy´ah ikiwa sio katika Uislamu ni ipi basi tofauti kati yake na Uislamu? Tunataraji kutoka kwako ubainifu wa wazi na wenye kukidhi kiu wenye kusapotiwa na dalili sahihi na khaswa madhehebu ya Shiy´ah na I´tiqaad zao na ubainishe baadhi ya mapote yaliyozushwa katika Uislamu.

[49] Uk. 266-267 fatwa 8852

Jibu: Madhehebu ya Shiy´ah al-Imaamiyyah ni madhehebu yaliyozushwa katika Uislamu kuanzia misingi na matawi yake. Tunakuusia kurejea kitabu "al-Khutwut al-´Ariydhwah", "al-Mukhtaswar at-Tuhfah al-Ithnaa ´Ashriyyah", "Minhaaj-us-Sunnah" ya Shaykh-ul-Islaam. Humo mna ubainifu mwingi juu ya Bid´ah zao.[50]

119. Maana Ya Bid´ah Na Baadhi Ya Mifano Yake

Swali 119: Tunaomba mtuwekee wazi ni nini Bid´ah na aina zake?

Jibu: Bid´ah ni ´ibaadah ambazo hazikuweka Allaah. Kama mfano wa kusherehekea Maulidi, usikuwa Israa´ na Mi´raaj, muadhini kunyanyua sauti kwa kumswalia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) baada ya kumaliza kutoa adhaana na mfano wa hayo. Kuna wanachuoni waliotunga vitabu kuhusu Bid´ah na aina zake. Tutaelekeza katika baadhi yavyo:

1- Kitaab-us-Sunan wal-Mubtada´aat cha Shaykh Muhammad Ahmad ´Abdis-Salaam al-Hawaamidiy.

2- Kitaab-ul-Ibdaa´ fiy Madhwaar-il-Ibtida´aah cha Shaykh ´Aliy al-Mahfuudhw.

Vyote viwili ni vya wanachuoni wa Misri. Kabla yavyo kwa muda mrefu kuliandikwa kitabu "al-Bid´ah wan-Nahiy ´anhaa" cha Imaam Muhammad bin al-Wadhdhwaah na kitabu "al-I´tiswaam" cha ash-Shaatwibiy.[51]

[50] Uk. 268 fatwa 9420

[51] Uk. 327 fatwa 3230

120. Anayelingania Katika Sunnah Anaitwa Kuwa Ni Mfitinishaji?

Swali 120: Kuna wenye kusema ni wajibu kwa mtu kuepuka kuzungumzia Bid´ah na Sunnah. Mwalimu akizungumzia juu ya mambo haya anatumbukia katika matatizo na watu wengine kwa sababu watu wengi ni wazushi na hawajui ni nini Sunnah. Kwa ajili hiyo mtu anatumbukia katika migogoro pamoja nao. Hivyo fitina inazuka kwa vile watu hawayakubali mafunzo haya kwa kuzingatia ya kwamba yanaenda kinyume na matamanio yao. Je, mwenye kusahihisha ´Aqiydah kwa kuisafisha na Bid´ah anaitwa "mfitinishaji" au yule mwenye kwenda kinyume na maamrisho ya Allaah ndiye ambaye anasababisha fitina?

Jibu: Mlinganizi anatakiwa kuwa mjuzi juu ya yale anayolingania na yale anayokataza, mwenye hekima juu ya yale anayoamrisha na yale anayokataza. Vilevile anatakiwa kupima kati ya manufaa; atangulize yale yenye manufaa zaidi juu ya yale yasiyokuwa na manufaa sana. Sambamba na hilo aangalie madhara na kutanguliza yale yenye madhara kidogo ili kuepuka makubwa zaidi. Manufaa na madhara yote mawili yakikutana na manufaa yakawa na nguvu zaidi ayatendee kazi. Na madhara yakiwa ndio ambayo yana nguvu basi asifanye kitu.

Kujengea juu ya hilo anatakiwa kuithibitisha Sunnah na kuibainisha na akemee Bid´ah na kuwabainishia nayo watu. Lakini hata hivyo anatakiwa kufanya hayo kwa hekima, maneno mazuri na kuzungumza kwa njia ilio nzuri. Amesema (Subhaanahu wa Ta´ala) katika Qur-aan:

ادْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ

"Waite [watu] katika njia ya Mola wako kwa hikmah na mawaidha mazuri na jadiliana nao kwa ambayo ni mazuri zaidi." (16:125)

Kwa kufanya hivyo hatoitwa kuwa ni mfitinishaji.[52]

121. Kusoma Qur-aan Kwa Pamoja Baada Ya Swalah Za Faradhi

Swali 121: Katika ada yetu sisi watu wa Marocco tunasoma Qur-aan kwa pamoja asubuhi na jioni baada ya swalah ya asubuhi na maghrib. Kuna wanaosema kuwa ni Bid´ah.

Jibu: Kulazimiana na kusoma Qur-aan kwa pamoja kwa sauti ya pamoja baada ya kila swalah ya asubuhi na maghrib au nyinginezo ni Bid´ah. Hali kadhalika kulazimiana na kuomba du´aa za pamoja baada ya swalah. Ama kila mmoja akisoma kivyake au wakafundishana Qur-aan kwa njia ya kwamba kila anapomaliza mmoja mwingine na yeye anasoma na wakamsikiliza, hii ni aina bora ya ´ibaadah. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) anasema:

“Hawatokusanyika watu katika Nyumba miongoni mwa nyumba za Allaah, wakisoma Kitabu cha Allaah na wakidurusishana nacho isipokuwa huteremkiwa na utulivu, hufunikwa na rahmah, Malaika huwazungumza na Allaah anawataja kwa wale walio Kwake.”[53]

[52] Uk. 336-337 fatwa 4250

[53] Uk. 342 fatwa 4994

122. Kusoma Qur-aan Kwa Pamoja Siku Ya Ijumaa

Swali 122: Ni ipi hukumu ya kusoma Qur-aan kwa pamoja kwa sauti moja na khaswa siku ya Ijumaa kabla ya imamu kuingia?

Jibu: Haijuzu kufanya hivo. Jengine ni kuwa kukhusisha hilo siku ya Ijumaa kabla ya imamu kuingia ni Bid´ah iliyozushwa.[54]

123. Kukusanyika Kusoma Qur-aan Kwa Ajili Ya Kupata Baraka Kazini

Swali 123: Je, inajuzu kwa mtu kuwakusanya watu na akawaamrisha kumsomea Qur-aan kwa lengo moja wapo kama mfano wa kubadilisha kazi na akawakusanya watu wamsomee Qur-aan ili aweze kufikiwa na baraka katika kazi yake?

Jibu: Allaah ameteremsha Qur-aan ili watu waabudu kwa kisomo chake na kutendea kazi hukumu zake na iwe ni miujiza kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kitendo hichi ulichotaja sio miongoni mwa mambo yaliyoweka Allaah (Subhaanah).[55]

[54] Uk. 342-343 fatwa 6364

[55] Uk. 343 fatwa 9697

124. Kualika Watu Wasome Qur-aan Ili Mtu Anyookewe Na Mambo Yake

Swali 124: Uganda mtu akitaka kumuomba Mola Wake amkunjulie riziki anawaalika baadhi ya wasomi wanahudhuria kwake na kila mmoja anakuja na msahafu wake na wanaanza kusoma; mmoja anasoma Yaasiyn kwa kuwa ndio moyo wa Qur-aan, wa pili al-Kahf, wa tatu al-Waaqi´ah, ar-Rahmaan, ad-Dukhaan, al-Ma´aarij, Nuun, al-Mulk, Muhammad, Fath au nyinginezo katika Suurah za Qur-aan. Hawasomi al-Baqarah wala an-Nisaa´. Baada ya hapo wanaomba du´aa. Je, mfumo huu umewekwa katika Uislamu? Ikiwa haukuwekwa tunaomba utueleze mfumo uliyowekwa katika Shari´ah pamoja na dalili.

Jibu: Kusoma Qur-aan pamoja na kuzingatia maana yake ni katika ´ibaadah bora. Kumuomba Allaah du´aa, kurejea Kwake juu ya kufanikiwa katika kheri, kukunjuliwa riziki na kheri nyenginezo ni ´ibaadah iliyowekwa.

Lakini kusoma Qur-aan kwa sura iliyotajwa katika swali ambapo kunagawiwa Suurah maalum kwa watu wengi kutoka katika Qur-aan na kila mmoja anasoma Suurah yake na baada ya hapo kuomba du´aa ya kukunjuliwa riziki na kadhalika ni Bid´ah. Hili halikuthibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) si kwa njia ya maneno wala vitendo. Vilevile halikuthibiti kutoka kwa Swahabah yeyote (Radhiya Allaahu ´anhum) na maimamu wa Salaf (Rahimahumu Allaah). Kheri inapatikana kwa kuwafuata Salaf na shari inapatikana kwa waliokuja nyuma kuzua. Imethibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

“Mwenye kuzua katika dini yetu hii yasiyokuwemo basi atarudishiwa mwenyewe.”

Kumuomba Allaah du´aa ni jambo limewekwa katika nyakati zote, sehemu zote na katika hali zote sawa za shida na raha. Miongoni mwa sehemu ambazo Shari´ah imekokoteza kuomba du´aa ni katika Sujuud wakati wa swalah, wakati wa daku na mwisho wa swalah kabla ya kutoa Salaam. Imethibiti ya kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Mola Wetu hushuka katika mbingu ya dunia kila usiku kunapobaki thuluthi ya mwisho na anasema: “Ni nani mwenye kuniomba du´aa nimuitikie? Ni nani mwenye kuniomba nimpe? Ni nani mwenye kuniomba msamaha nimsamhe.”

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

Ibn ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) amesimulia ya kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Katika Rukuu´ muadhimisheni Mola na katika Sujuud jitahidini kwa du´aa.”

Ameipokea Ahmad, Muslim, an-Nasaa´iy na Abu Daawuud.

Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) amesimulia kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Mahali ambapo mja anakuwa karibu na Mola Wake ni pale anapokuwa amesujudu. Hivyo kithirisheni du´aa.”

Ameipokea Muslim, Abu Daawuud na an-Nasaa´iy.

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Ibn Mas´uud (Radhiya Allaahu ´anh) ambaye ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) baada ya kumfunza Tashahhud akamwambia:

“Kisha una khiyari ya kuomba du´aa uitakayo ambayo itaitikiwa.”[56]

[56] Uk. 345-346 fatwa 4028

125. Kusoma Qur-aan Ijumaa Kabla Ya Imamu Kuingia Ni Bid´ah

Swali 125: Je, ni halali msomaji akasimama siku ya Ijumaa kabla ya imamu kuja na akija msomaji anakaa na baada ya hapo Khatwiyb anatoa Khutbah? Je, ni miongoni mwa adabu za Ijumaa na Sunnah zake au ni katika Bid´ah munkari?

Jibu: Hatujui dalili yenye kufahamisha msomaji akasimama na kusoma Qur-aan siku ya Ijumaa kabla ya imamu kuingia na watu wakamsikiliza na imamu akiingia msomaji anaacha kusoma. Asli katika ´ibaadah ni kukomeka (Tawqiyf). Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kufanya kitendo kisichokuwa ndani yake dini yetu, basi atarudishiwa mwenyewe.”

Ameipokea Muslim katika “as-Swahiyh” yake.[57]

126. Kukhusisha Kufanya Matendo Maalum Rajab

Swali 126: Kuna masiku kunafungwa swawm ya kujitolea katika mwezi wa Rajab. Je, masiku hayo yanakuwa siku za mwanzo, katikati au mwishoni?

Jibu: Hakukuthibiti Hadiyth maalum juu ya fadhila ya swawm ya Rajab mbali na yale aliyopokea an-Nasaa´iy, Abu Daawuud na Ibn Khuzaymah akaisahihisha kupitia Hadiyth ya Usaamah aliyesema: “Nilimuuliza: “Ee Mtume wa Allaah! Hatukukuona unafunga mwezi wowote kama unavyofanya Sha´baan.” Akasema: “Huo ni mwezi ambao watu wengi wanaghafilika nao baina ya Rajab na Ramadhaan. Huyo ni mwezi ambao

[57] Uk. 357-358 fatwa 2775

matendo yanapandishwa kwa Mola wa walimwengu. Napenda matendo yangu yapandishwe hali ya kuwa nimefunga.”

Kumethibiti Hadiyth kwa jumla zinazokokoteza juu ya kufunga siku tatu kwa kila mwezi, kufunga masiku meupe kila mwezi; siku hizo ni 13, 14 na 15, kufunga miezi mitukufu na kufunga Jumatatu na Alkhamisi. Rajab inaingia katika jumla hiyo. Ikiwa ni mtu mwenye pupa kuchagua kufunga mwezi maalum basi afunge masiku matatu meupe au siku ya Jumatatu na Alkhamisi. Vinginevyo mambo ni sahali.

Kuhusiana na kukhusisha siku maalum kufunga Rajab hatujui kuwa kitendo hicho kina asli katika Shari´ah.[58]

127. al-Lajnah ad-Daaimah Kuhusu Swawm Rajab Na Sha´baan

Swali 127: Tumeona watu wanadumu kwa swawm katika Rajab na Sha´baan na katika muda huu wanafuatisha miezi hiyo kwa kufunga Ramadhaan pasi na futari. Je, kumethibiti Hadiyth juu ya hayo na ni zipi?

Jibu: Haikusihi kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuwa alifunga Rajab kikamilifu wala mwezi wa Sha´baan kikamilifu isipokuwa tu Ramadhaan. Vilevile hilo halikuthibiti kutoka kwa yeyote miongoni mwa Maswahabah zake (Radhiya Allaahu ´anhum). Bali haikuthibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba alifunga mwezi wowote kikamilifu isipokuwa Ramadhaan peke yake. Imethibiti kutoka kwa ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) ya kwamba amesema:

“Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa anafunga mpaka tunasema kuwa hatoacha kufunga na anaacha kufunga mpaka

[58] Uk. 363 fatwa 2608

tunasema kuwa hatofunga. Sikumuona Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akikamilisha mwezi wowote isipokuwa tu Ramadhaan na sikuona mwezi wowote akikithirisha kufunga sana kama katika Sha´baan."

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

Ibn ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) amesema:

"Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakupatapo kufunga mwezi kikamilifu mbali na Ramadhaan. Alikuwa anafunga mpaka anasema mwenye kusema ´hatoacha kufunga` na anaacha kufunga mpaka anasema mwenye kusema ´hatofunga`."

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

Kufunga kwa kujitolea mwezi mzima wa Rajab na Sha´baan ni jambo linaloenda kinyume na uongofu wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Sunnah yake. Hivyo ni Bid´ah iliyozushwa. Imethibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

"Mwenye kuzua katika dini yetu hii yasiyokuwemo, atarudishiwa mwenyewe."[59]

128. al-Faatihah Baada Ya Kuomba Du´aa Ni Bid´ah

Swali 128: Je, Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa anasoma al-Faatihah baada ya du´aa?

[59] Uk. 364 fatwa 5169

Jibu: Haikuthibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba alikuwa akisoma al-Faatihah baada ya du´aa kutokana na tunavyojua. Kusoma al-Faatihah baada ya kuomba du´aa ni Bi´ah.[60]

129. Kusoma al-Faatihah Kabla Na Baada Ya Mambo Mbali Mbali Ya ´Ibaadah

Swali 129: Ni ipi hukumu ya msemo "al-Faatihah juu ya roho ya fulani", "al-Faatihah Allaah atusahilishie jambo lile", baada ya kuzaliwa wanasoma al-Faatihah au baada ya kumaliza kusoma Qur-aan wanasema "al-Faatihah" na waliohudhuria pale wanasoma. Kadhalika desturi imezowea kusoma al-Faatihah kabla ya ndoa. Ni ipi hukumu ya hilo?

Jibu: Kusoma al-Faatihah baada ya du´aa, baada ya kumaliza kusoma Qur-aan au kabla ya ndoa ni Bid´ah. Hilo halikuthibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wala Maswahabah zake (Radhiya Allaahu ´anhum). Imethibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

"Mwenye kufanya kitendo kisichokuwa humo dini yetu atarudishiwa mwenyewe."[61]

[60] Uk. 376-377 fatwa 5881

[61] Uk. 384 fatwa 8946

130. al-Faatihah Baada Ya Swalah Za Faradhi

Swali 130: Je, ni katika Sunnah au inajuzu kusoma al-Faatihah baada ya swalah ya faradhi sawa mtu kivyake au kwa pamoja?

Jibu: Kusoma al-Faatihah baada ya faradhi, sawa mtu kivyake au kwa pamoja, sio katika Sunnah.[62]

Endelea na mjaladi wa tatu...

[62] Uk. 384 fatwa 9509